GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. 256 | R/Akhir-Jum/Awwal 1447 AH | Oktoba– 2025 | Tabook 1404 HS | BEI TSH 800/=

WAHITIMU - SHULE YA MSINGI AHMADIYYA WAFANYA MAHAFALI YAO

Na.
Sheikh Abid Mahmood Bhuti

Miongoni mwa taasisi muhimu sana katika jumuiya ya Waislamu waahmadiyya hapa nchini ni shule ya msingi na chekechea iitwayo *"Ahmadiyya pre/primary school,"* iliyopo Kihonda katika Manispaa ya Morogoro.

Shule hii ya Engish medium ilianzishwa takribani miaka 12 iliyopita na hadi sasa imepiga hatua kubwa chini ya uongozi wa Maulana Sheikh Abid Mahmoud Bhatti sahib.

Mnamo siku ya jumamosi ya tarehe 30 August 2025 yalifanyika mahafali ya kuwaaga wahitimu wa darasa la saba wanao tarajia kufanya mitihani yao tarehe 10-11 september mwaka huu.

Hafla hiyo ilifanyika katika ukumbi wa shule uitwao *"Masroor hall"* uliopo shuleni hapo. Mgeni rasmi katika hafla hiyo Alikuwa ni Maulana Sheikh Khawaja Muzaffar sahib Amir na Mbashiri Mkuu hapa Nchini. Pia wageni mbalimbali waalikwa walishiriki katika hafla hiyo wakiwemo wazazi/



walezi wa wahitimu, Sheikh wa Jamaat Ahmadiyya Mkoa wa Morogoro, Afisa Elimu kata ya Kihonda Maghorofani n.k

Hafla ilianza majira ya saa 4:30 asubuhi kwa usomaji wa Qur'an Tukufu na kufuatiwa na ripoti ya shule iliyosomwa na Mwalimu Mkuu wa shule. Katika ripoti yake Mwalimu Mkuu alieleza

UK. 09

HATIMA YA WAPINZANI WAWILI WA SEYYIDNA AHMAD[AS]

(SH. MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII NA ABDULLAH ATHAM)

BISHARA YA MASIH AS KUMHUSU ABDULLAH ATHAM

Bishara hii inayomuhusu Abdullah Atham ni ishara kwa wakristo kwa ujumla na hususa Wakristo wa Bara Hindi. Sijui msomaji mpenzi wa makala hii, kama unafahamu mashambulio mabaya sana yaliyofanywa na wahubiri wa kikristo siku hizo kinyume cha tabia ya Mtume Mtukufu

UK. 05

AHMADIYYA NA HISTORIA YA ZANZIBAR

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Makala ya kusisimua katika gazeti la Mapenzi ya Mungu iliyoandikwa na ndugu yetu Ally Khamisi Juma maarufu kwa lakabu ya 'Majani' kuhusu historia ya Ahmadiyya katika visiwa vya Marashi ya karafuu Zanzibar imenipa hamu na kwa hakika imenionjesha asali tamu ya historia ya kisiwa hicho maarufu katika Bahari ya Hindi. Ni Makala ambayo imenikumbusha mambo ambayo Inshallah yatasaidia kutupa mwanga zaidi kuhusu Uhusiano wa Ahmadiyya na Zanzibar.

Kuna haja kubwa ya kuendeleza utafiti kuhusu Masahaba watakatifu wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] ambao wanaaminika kuwa walikuwa katika

UK. 03

MAJIBU KWA MASALAFI UK. 04

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

WITO WA KHALIFATUL MASIHI V^atba

Katika mwaka 1920 kiongozi wa Jumuiyya ya Ahmadiyya Duniani Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad^ra alitoa wito kwa wazazi wa Kiahmadiyya wawatoe Watoto wao ili wakaeneze na kutetea Islam katika pembe zote za Dunia watakakotumwa.


Wito huu unatakiwa tukae chini na kutafakari hadi hivi leo. Inawezaje kuwa rahisi kwa mtu kutoa mwanae na akamruhusu aende mahala asipopajua na kule ambako hajawahi kufika. Imani ya namna hii inakujaje na inapatikana vipi. Si jambo rahisi hata kidogo. Ni rahisi kulisikia katika hadithi na maelezo lakini gumu likikufika. Kumbe jambo hili lilikuwa rahisi kutokana na maelezo ya kina na ufafanuzi alioutoa Khalifatul Masih -II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad^ra kuhusu dhabihu aliyoitoa Hadhrat Nabii Ibrahim^as kwa mwanae Ismail^as.

Tukio la Nabii Ibrahim^as halina mfano katika historia ya binadamu. Ni tukio la aina yake. Yanayoendelea hivi leo Duniani kwa kiwango kikubwa yanaweza kunasibishwa na baba huyu wa Mitume. Wewe ukisikia kuwa Mtume Muhamad^saw anasema; "Yeye ni matunda ya dua ya Nabii Ibrahim^as" Je hapo kuna cha kuuliza tena. Mataifa makubwa mawili, Waarabu na Waisraeli yananasibishwa na Nabii Ibrahim^as hivi unahitaji Ushahidi gani tena kuhusu rafiki huyu wa Allah.

Wazee hao walielewa vizuri tukio la Nabii Ibrahim^as la kumtoa mwanae wa pekee wakati ule Hadhrat Ismail^as ili kutimiza amri na matakwa ya Allah. Nabii Ibrahim^as alitumia miaka mingi akimuomba Allah Ampatie mtoto. Toka ujana wake kilio chake kilikuwa ni hicho. Alikuwa na umri wa miaka 90 na maombi yake yakakubaliwa na kumpata Hadhrat Ismail^as jina ambalo maana yake ni kwamba "Maombi yamekubaliwa". Ni furaha na utulivu wa moyo kupokelewa dua baada ya miaka mingi ya vilio. Kabla hata furaha hiyo haijaisha unapewa amri ya kwamba umtoe dhabihu huyo mtoto. Mtoto anaulizwa juu ya jambo hilo na anajibu; "Timiza yote uliyoambiwa na Mola wako". Akiwa safarini Kwenda kutimiza hilo anaambiwa; "Basi umekwishatimiza azma yako". Wazee hao waliokuwa wanamsikiliza kiongozi wao wa kiroho wakaelewa vizuri la kufanya na kuwatoa Watoto wao ambao wamefanya kazi kubwa katika sehemu nyingi Duniani.

Mwito huo wa Hadhrat Khalifatul Masih-II^ra ulifika kwetu Afrika na kwa kiwango kikubwa ukatimizwa. Hapa Tanganyika ni jambo la kutia moyo kwamba mwaka 1955 mzalengo mmoja mjini Tabora alimtoa mwanae wa umri wa miaka 13 kwenda Rabwah Pakistan kupata elimu ya dini na hatimaye kuitumikia Jamaat. Kijana huyo alimaliza masomo yake na kuja kuitumikia Jamaat ya Ahmadiyya Tanzania. Yeye amejizolea sifa ya kuwa Sheikh aliyeitumikia Jamaat kwa miaka mingi zaidi kuliko Sheikh yeyote Duniani. Na hili hatulisemi kwa kujinaki Mwenyezi Mungu Apishe mbali bali tunatoa shukrani kwani tumeambiwa; "Neema za Mola uzidhihirishe".


Tukio hili la Nabii Ibrahim^as lilikuwa somo kwa wazee waliopita na linaendelea kuwa somo kwetu sisi sote. Hakuna maendeleo ya aina yoyote yanayoweza kutokea bila kuwepo na watu ambao wako tayari kujitolea. Hakuna maendeleo bila ya watu ambao wanapata maumivu ili wengine waweze kupata afueni. Ni Dhahiri ya kwamba sisi tunaposherehekea Eid-Ul-Adh'ha hakuna miongoni mwetu ambae alishiriki katika lile jaribio alilopewa Nabii Ibarahim^as. Tunao wajibu mkubwa wa kuwatoa wa akina Ismail tulio nao tukikumbuka ya kwamba tuwe tayari kutoa kilicho bora na kilicho bora tu ndicho kinamfikia Allah. Allah atusaidie katika kutimiza hilo. Ameen.



QUR'AN TUKUFU

ذٰلِكَ ۚ وَمَنْ يُّعَظِّمْ حُرُمٰتِ اللّٰهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهٗ عِنْدَ رَبِّهٖ ؕ وَاُحِلَّتْ لَكُمُ الْاَنْعَامُ اِلَّا مَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْاَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوْا قَوْلَ الزُّوْرِ ۙ﴿۳۱﴾

Huu ni mwongozo wa Allah; na anayevitukuza vitu vitakatify vya Allah, basi hiyo ni heri kwake mbele ya Mola wake. Na mmehalalishiwa wanyama isipokuwa wale mnaosomewa; basi jiepusheni na ucafu wa masanamu na jiepusheni na kusema uongo. (22:31)



NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hazrat Abdurrahman bin Abi Bakrah (ra) ya kwamba Mjumbe wa Allah (saw) alisema: Je, niwaambieni kuhusu madhambi makubwa? Tukusema: Naam, ewe Mjumbe wa Allah. Akasema: Kumshirikisha mwingine na Allah; na kuwaasi wazazi. Wakati huo alikuwa ameegama basi akakaa sawasawa na akasema: Sikilizeni, mjiepushe na kusema uongo na kutoa ushuhuda wa uongo; na akaendelea kukariri maonyo hayo hata nikafikiri hataacha kusema. (Bukhari)



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa^as

"basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na maneno yote ya uongo. Hii inaonyesha kuwa uongo nao ni sanamu na yule anayetegemea uongo huwa anaacha kumtegemea Mwenyezi Mungu. Hivyo basi, kwa kusema uongo mtu humwacha Mungu." (Hekima ya Mafundisho ya Kiislam, uk. 75) "Leo hali ya dunia inasikitisha sana. Popote unapoona unawapata mashahidi wa uongo. Kufungua kesi za uongo halichukuliwi kuwa jambo zito—hata shahada na vyeti vya elimu vinaghushiwa. Watu wakifanya mazungumzo huwa wanaacha ukweli makusudi. Hivyo, mimi ninawauliza wale wanaodhani hakuna haja ya jumuiya hii: Je, huu ndio Uislamu uliofundishwa na Mtume Muhammad (saw)? Mwenyezi Mungu Amesema kuwa uongo ni uchafu na mtu anapaswa kuepukana nao… Ameuweka uongo sawa na ushirikina. Kama vile mtu asiyejua anainama mbele ya sanamu kwa kumwacha Mwenyezi Mungu. Vivyo hivyo, kwa kuacha ukweli, mtu huyafanya maneno ya uongo kuwa sanamu ili kufanikisha makusudio yake. Hii ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Ameuweka uongo sawa na ushirikina na kueleza mfanano huo. Kama vile mshirikina anavyoomba dua kwa sanamu, vivyo hivyo mtu mwongo hufinyanga sanamu kwa ajili yake na anadhani kuwa atasalimika kwa sababu yake. Ni uchafu ulioje! Wakiulizwa: 'Kwa nini mnajiingiza katika ushirikina huu? Jiepusheni na uchafu huo!' Wanajibu: 'Kwa nini tuuache? Hatuwezi kuishi bila ya uongo.' La kusikitisha sana kuwa wanajenga kila kitu juu ya msingi wa uongo? Lakini ninawahakikishia kwamba hatimaye ukweli utashinda. Kila baraka na wema hupatikana kutokana na ukweli." ***(Malfuzat, juzuu 8, kur. 349-350)***

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Aziz Ahmad Ng'amilo
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Sheikh Shahab Ahmad.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

AHMADIYYA NA HISTORIA YA ZANZIBAR

Kutoka uk. 01

jeshi la Muingereza lililotumwa katika visiwa hivyo kumsaidia Sultani aliyekuwa anakabiliwa na maasi. Inasemekana kuwa Masahaba hao baada ya muda wao wa kazi waliingia mitaani nakuanza kuhubiri ujaji wa Masihi na Mahadi. Kipande hiki muhimu cha Historia kinatakiwa kifanyiwe utafiti wa kina kwa msaada wa Wanahistoria walioko Qadain, Rabwah na London. Katika miaka ya 1930, 1940 hadi 1960 vijana wa visiwa vya Unguja na Pemba walikuwa Mashabiki wakubwa wa Jumuiyya ya Ahmadiyya. Kwa ujumla visiwa hivyo vilikuwa bustani iliyoruhusu maua ya kila aina yachanue bila kikwazo na kweli (Zanzibar ni njema atakae aje).

Sote tunakumbuka kwamba visiwa hivi vilikuwa chem chem ya dini ya Islam katika ukanda huu wa Afrika. Elimu yako ya dini ilikuwa na walakini kama hujapanda meli na kuweka nanga Zanzibar. Kabaka Mwanga wa Buganda aliwatuma vijana wake Zanzibar kutoka katika Ufalme wake ili wapate elimu ya dini. Ikumbukwe hata elimu ya Magharibi ilipokelewa na vijana wengi na walikuwa wamekwenda katika vyuo mbalimbali duniani kupata elimu. Usione ajabu kuona ya kwamba visiwa hivi vimetupatia wasomi wengi majina maarufu ni Pamoja na Alhaji Abudu Jumbe, Alhaji Alli Hassani Mwinyi, Kassim Hanga, Profesa Sharif, Profesa Saada Yahya Othman, Profesa Harubu Othman, Abdallah Balozi, Salim Ahmed Salim ambaye bila vitimbwi vya Marekani angelikuwa Katibu Mkuu wa Kwanza Mwafrika wa Umoja wa Mataifa, Mwandishi maarufu wa riwaya wa kwanza kutoka Afrika Mashariki ambae ni Mzanzibari kindakindaki Abdulrazak Gurna.

Mawazo ya kimapinduzi yalipokelewa katika visiwa hivyo kutokana na harakati za Ghamal Abdulnassir zilizomo katika kitabu chake "Philosophy of the Revolution" Mawazo hayo yalienea katika vijiwe vingi vya Zanzibar. Fikra za Karl Marx 'Directical materialism na Historical materialism' zilizoenezwa na Profesa Abdulrahman Mohammed Babu ambae aliishi wakati wa ukombozi na mapinduzi. Kipindi baada ya vita ya pili 1939 -1945 Dunia ilitawaliwa na kile Mwenyekiti Mao -Tse-Tung wa China alichokiita; "Nchi zinataka uhuru, mataifa yanataka ukombozi na watu wanataka mapinduzi". Wana Mapinduzi wakashika kalamu ili kueneza silaha ya itikadi. Jawalal Nehru wa India akiwa gerezani alimwandikia binti yake "Glimpse of world History", Flantz Fanon aliandika "The Wretched of the Earth', Kwame Nkurumah akaandika "Neo-Colonialism, The last stage of imperialism" Rene Dumont – "False start in Africa". Profesa Babu nae hakuwa nyuma, akaandika African Socialism or Socialist Africa? Visiwa hivi vilikuwa visiwa vya Mawazo na sifa yao kubwa ilikuwa mahaba yao ya kusoma.

Ni mapenzi hayo ya kupenda kusoma bila kubagua au kuchagua yaliyowafanya vijana hao wa visiwani wakutane na maandishi ya Jumuiyya ya Ahmadiyya. Maandishi hayo waliyapokea kwa furaha kwani yalikuwa yanawakilisha maoni yao na matumaini yao. Mwaka 1936 Sheikh Mubarak Ahmad alitoa waraka uliokuwa unatoa wito wa kuheshimiwa kwa watu wote bila ya ubaguzi sio kutokana na nasaba au mali ila mtu aheshimiwe kwa sababu ni binadamu. Na heshima inatokana na usafi wa moyo. Aliwakumbusha katika waraka huo kuwa ubora wa mtu ulitokana na Ucha Mungu sio rangi yake ambayo hakufanya juhudi yoyote kuipata. Wazo hili lilipewa msisitizo zaidi na Mwimbaji maarufu wa Zanzibar Siti binti Sadi alipoimba;

Si bora uzuri
Na sura jamala
Kuwa mtukufu
Na jadi kubeli
Hasara ya mtu,
Kukosa akili.

Gazeti la Mapenzi ya Mungu lilivamiwa kwa mapenzi na jazba kubwa kama vile Wahaya wanapovamia senene. Utetezi wa gazeti hili kwa wanyonge lilianikiwa kuwapata mashabiki lukuki na likawa kiini cha mazungumzo katika vijiwe vya kahawa. Tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kiswahili ilipotoka mwaka 1953 ilipokelewa kwa heshima na furaha kubwa. Sultani wa Zanzibar aliwakaribisha kwa taadhima wawakilishi wa Ahmadiyya waliofika katika Kasri yake kumkabidhi tafsiri ya Qur'an Tukufu kwa Kiswahili. Ujumbe huo uliongozwa na Sheikh Mubarak Ahmad akiwa Pamoja na Mwalimu Akhtar Ayyaz na Mwalimu Kaluta Amri Abedi.

Jambo alililigundua kwa haraka Sheikh Mubarak Ahmad ni ghadhabu waliyokuwa nayo vijana wa Unguja kutokana na madhila waliyokuwa wanapitia. Na hii ilitokana na kutofahamu vuzuri historia ya Islam. Mafundisho sahihi ya Islam yanatofautisha baina ya mafundisho yenyewe na vitendo vya watu. Ni Bahati mbaya kwa hao waliofikiri kuwa Islam ni milki yao na wapo watu wa Daraja la tatu. Sheikh Mubarak Ahmad Aliona tatizo lao la msingi ni kutofahamu historia ya Islam na hali ya kujiona wanyonge. Katika hayo mawili, aliwaamsha kwa kutoa maelezo yaliyofuta kujiona wanyonge na watu wa hali ya chini. Dawa aliyokuwa nayo ni kuzama katika historia ya Islam.

Historia inaonesha ya kwamba waliopokea mwanzoni Islam mjini Maka walikuwa wanyonge na dhalili na hivyo kimsingi Islam ni sauti ya wanyonge na imekuja kuwakomboa wanyonge. Siku za mwanzo za Islam Mwana wa Afrika aliteswa kwa ajili ya Islam. Hakuna pia anayebisha kuwa Bi. Hajira alitoka Afrika kwa hiyo ni Mwafrika. Ni mtoto kutoka katika ukoo wa Kifalme. Nabii Ibrahim alimuoa na kujaliwa kupata mwana aitwaye Ismail na Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni kizazi cha Ismail. Tizama mama huyu alivyoonesha kwa vitendo maana halisi ya neno Istiqama. Yeye na mwanae huko jangwani hakuna maji wala chochote Nabii Ibrahim anawaacha huko na suala analouliza huyo mama ni kwamba; kwa nini unatuacha hapa, Nabii Ibrahim anaonesha juu kwa ishara, mama huyo wa Imani katu hakati tamaa kati ya vilima vya Safaa na Marwa na pale alipomuacha Ismail anakuta chemchem ambayo hadi hivi leo inatoa maji yanayoitwa Zamzam. Kutokana na upatikanaji wa maji taratibu mji ukakua. Na ni katika mji huo Nabii Ibrahim (as) na Hadhrat Ismail (as) walipoamsha nguzo za nyumba ya kwanza kwa ajili ya kumuabudu Allah. Historia hii iliyotukuka unawezaje kuieleza bila kumnasibisha Bi. Hajira ambae ni mama kutoka Afrika? Unawezaje kujiita mnyonge unapopitia historia hii ya kusisimua na kujijengea kujiamini? Hakuna udhaifu mkubwa kuliko ule wa kutofahamu historia yako na kasumba hii imejengwa makusudi ili tujidharau sisi wenyewe na kujiona kuwa hatuna thamani yoyote.

Matukio hayo mawili ya Bi. Hajira (ra) na Hadhrat Bilal (ra) yanatupa ujumbe wa aina mbili; kwa upande wa Bi. Hajira ni uvumilivu wa hali ya juu na kwa upande wa Bilal kuwaita binadamu kwenye aliyoileta Allah. Kila siku inatolewa adhana na daima inatukumbusha sauti ya Hadhrat Bilal ya sisi Kwenda kumuabudu Aliyetuumba. Na kuna adhana gani nzuri kuliko ile ya Hadhrat Bilal? Hadhrat Bilal (ra) alikuwa miongoni mwa Masahaba maarufu wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliyesimama kutetea Islam. Yeye anakumbukwa kwa kuwa Muadhini wa kwanza wa Mtukufu Mtume Muhamamd (saw). Baadhi ya hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) zinanasibishwa naye. Wakati wa ushindi wa Maka, Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alitangaza kuwa, anayetaka kunusurika hivi leo aje chini ya bendera ya Hadhrat Bilal (ra). Khalifa wa pili wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw), Seyidna Umar bin Khatwab (ra) alimpata Hadhrat Bilal (ra) lakabu ya "Seyyid". Waafrika wanawezaje kujiona wanyonge? Hata wakati wa mateso na hiyo ni kabla ya hijra, Mtukufu Mtume Muhammad (saw) aliwashauri baadhi ya Masahaba wakapate hifadhi Uhabeshi. Mfalme wa kule 'Najashi' alikuwa muadilifu akawapa uhuru wa kukaa na kuabudu. Fitna zilitoka Maka kwamba Waislam wanamkashifu Nabii Isa (as) masingizio hayo yalijibiwa kwa hoja na Waislam wakaendelea kufaidi uhuru wa kuabudu. Zipo Habari ambazo hazijathibitishwa kihistoria kwamba ile mashua iliyokuwa imembeba Seyidna Athumani na mkewe Kwenda Uhabeshi ilitua Zanzibar kwani ilikuwa imepotea njia na baadae wakaanza safari ya Kwenda Uhabeshi.

Sheikh Mubarak Ahmad aliendelea kuchimba historia ya Islam na akawaeleza kuwa hata kabla ya Islam, enzi hizo zinazoitwa Jahiliya, washahiri wengi wa enzi hizo walikuwa Waafrika waliyopewa lakabu ya 'Aghribul al famme' (kunguru Weusi). Miongoni mwa hao ni Antaba Abe alizaliwa na mama wa Kihabeshi aliyeitwa Zabiba, huyu alishiriki katika harakati za 'Dakka' (vita vya Dakkaa). Licha ya utunzi wa mashairi alikuwa mpiganaji mzuri. Mashairi yake yanakubaliwa kuwa bora. Na hata wakati wa Islam mashairi yake yaliendelea kupendwa. Ammar bin Yassir alikuwa akishiriki vita vyote, na Khalifa wa pili Hadhrat Umar (ra) alimteua kuwa Gavana wa Kuff na zipo hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (saw) zinanasibishwa na yeye. All-Mukidau bin Ashuwaa alikuwa askari shujaa wa Islam. Akina mama wa kiafrika pia hawakuwa nyuma. Ummi Aymani Bakak alimlea Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alipokuwa mdogo.

Itaendelea toleo lijalo …. Insha Allah.

MAJIBU KWA MASALAFI

Kutoka Uk wa 1..

SURA YA SABA
BISHARA YA NABII ISA[AS]

Abu Halima ameendelea na ulalamishi wake na kuizungumzia Aya ya 7 ya sura Assaff kwa kesema

"(Makadiyani wamevuka mipaka juu ya Mtume (saw) kwa kuidai kwamba Mtume aliyetabiriwa na Isa ndani ya Qur-ani ni Ghulam Ahmad , wala si Mtume Muhammad(saw) " (ukurasa wa 14)

Naam ilivyo ni hivi :

Aya yenyewe inasema :

" NA ALIPOSEMA ISA BIN MARYAM ENYI WANA WA ISRAELI , MIMI NI MTUME WA ALLAH KWENU , NISADIKISHAYE YALIYO MBELE YANGU KATIKA TAURAT , NA KUTOA HABARI NJEMA YA MTUME ATAKAYEFIKA NYUMA YANGU JINA LAKE NI AHMAD "

Aya hii ina sehemu tatu .

i)Nabii Isa a.s anawambiya Mayahudi kwamba yeye ni Mtume kwao . Sehemu hii haina ubishi .

ii) Anasadikisha yaliyomo katika Taurat kwamba ni kweli . Je kwenye Taurat kuna nini ambalo Allah anatukumbusha hata sisi waislamu ?

Jawabu ni kwamba katika sura A'raf Allah sw anasema

" AMBAO WANAMFUATA MTUME , NABII ALIYE UMMI , AMBAYE WAO HUMKUTA AMEANDIKWA KWAO KATIKA TAURAT NA INJILI ....."

(Sura A'raf 7: 158)

Bila shaka ndugu msomaji umeelewa kwamba Mtume huyo ndiye Muhammad saw mwenye sifa ya " ummi " ametajwa ndani ya Taurat, NA Yeye Nabii Isa a.s anasadikisha kwamba ni kweli , katika ile Aya ya 61:7.

iii) Sehemu ya tatu ya Aya inasema (WAMUBASHIRAN) yaani Nabii Isa a .s anatoa habari njema na mpya kabisa ya Mtume mwingine ambaye hakutajwa kwenye Taurat , ambaye jina lake ni AHMAD . Siku zote neno BISHARA lina maana ya habari mpya na mifano ipo katika Kur-ani.

a) " MARA MALAIKA WAKAMNADIA HALI AMESIMAMA AKISALI CHUMBANI YAKWAMBA ALLAH ANAKUPA HABARI NJEMA YA YAHYA ....."
(Sura Aali- Imran, 3: 40)
Hii ilikuwa habari mpya kwa Nabii Zakariya a. s

b) "WALIPOSEMA MALAIKA EWE MARYAM , BILA SHAKKA AALAH ANAKUPA HABARI NJEMA ZA NENO LITOKALO KWAKE . JIN LAKE MASIHI ISA MWANA WA MARYAMU ....."
(Sura Aali Imran , 3 : 46)
Hii ilikuwa ni habari mpya kwa Maryam .

c) Bishara ya tatu ni bishara ya kuzaliwa Nabii Ismail : "WAKASEMA USIOGOPE , KWA YAKINI SISI TUNAKUPA HABARI NJEMA YA MTOTO MWENYE ELIMU "
(Sura Al – Hijri , 15 : 54)

Hii ilikuwa ni habari mpya kabisa kwa NABII Ibrahim a. S .

Hivyo BISHARA ya Isa a .s iliyomo katika aya ya 7 ya Sura Assaf , ni habari mpya ambayo haijatajwa wazi wazi ndani ya Taurat , na ndio maana pasipo shaka huyo ni mtu mwengine minghairi ya Mtume Muhammad (s.a.w)

Allah s.w anamaliza Aya hiyo 61 : 7 kwa kusema :

" LAKINI ALIPOWAFIKIA KWA ISHARA ZILIZO WAZI , WAKASEMA : HUU NI UDANGANYIFU DHAHIRI "

Basi yametimia ,wale Wayahudi ambao Nabii Isa a.s aliongea nao, Wameyasema hayo hayo kwamba huu ni udanganyifu dhahiri ,

Na Abu Halima pamoja na mashekhe wake wamejiunga nao . Na Mtume saw aliisha sema jambo hili . Akasema kwamba . mtazifuata desturi za wale wa kabla yenu shubiri kwa shubiri , dhiraa kwa dhiraa , hata kama waliingia katika shimo la kenge , basi nanyi mtawafuata humo.

Rejea : (Bukhari , kitabu – I'tiswam wassunnat)

Hivyo ndugu msomaji mpendwa usibabaishwe na watu wasiokuwa na elimu , watu waliotelekeza dini ambao kwa ajili yao , Allah s.w anamwambia Mtume s.a.w hivi :

"HAKIKA WALE WALIOFARAKANISHA DINI YAO , NA WAKAWA MAKUNDI MAKUNDI , HUNA UHUSIANO NAO WOWOTE "
(Sura Al- An'am , 6 : 160)

Mtume Muhammad (saw) jina lake hasa alilopewa wakati alipozaliwa ni Muhammad na maana yake ni " **mwenye kusifiwa sana "** na ilikuwa ni lazima aje Ahmad ambaye atamsifu sana Muhammad (saw), kwani Ahmad maana yake ni **"mwenye kusifu sana"** na huyo ndie Mirza Ghulam Ahmad ambaye alipewa jina Ahmad mara alipozaliwa .Mirza ni lakabu ya ukoo wake pamoja na Ghulam.

SURA YA NANE
NINI HUKMU YA KUMKATAA NABII WA ALLAH

Katika kijarida chake , Abu Halima ameandika ;

"Ukadiani ni ukafiri " (Ukurasa wa 16)

Ah hii ndio kawaida ya Waislamu wa sasa, kukufrishana ndio mtindo wa maisha yao , kama yeye anavyosema Uahmadiyya kwamba ni ukafiri , basi hata usalafi unasemwa hivyo hivyo .

Hebu soma haya :

" Mawahabi au kama wanavyojiita "Answar sunna" ni kikundi cha watu ambao wao wenyewe wanajiita Waislamu , lakini kwa hakika ni genge lililojiandaa na kusimama imara kabisa kuupiga vita Uislamu "

Rejea (Upotofu wa Madhehebu ya Uwahabi , uk 8)

Hatushangai kwani mtukufu Mtume s.a.w alishasema kwamba waligawanyika Mayahudi makundi 72 hivyo hivyo na watagawanyika Waisalamu makundi 73 na kila kundi litallani makundi mengine, lakini makundi yote hayo yote motoni isipokuwa moja . Alipoulizwa ni lilpi hilo lenye wokovu , alisema kwamba ni lile lenye hali yangu mimi na maswahaba zangu.

Rejea (Tirmidhii kitabul – Iman j.2 uk 89)

Ndugu msomaji , ukitaka kulijua hilo kundu , soma vizuri maneno ya Mtume s.a.w kwa kutafakari . Mtume s.a.w ameweka mizani kwamba waligawanyika Mayahudi makundi 72 na Waislamu watagawanyika makundi 73 . Hivyo ukitaka kulijua kundi lenye wokovu upande wa Wislamu , basi litafute kundi kama hilo upande wa Mayahudi . Utakuta kundi hilo ni lile la Wayahudi waliomwamini Nabii Isa a.s Allah s.w Anasema :

" ENYI MLIOAMINI KUWENI WASAIDIZI WA ALLAH , KAMA ALIVYOSEMA ISA BIN MARYAM KUWAMBIA WANAFUNZI WAKE , NI NANI MSAIDIZI WANGU KWA AJILI YA ALLAH ? WANAFUNZI WAKASEMA ; SISI NI WASIDIZI WA ALLAH . BASI TAIFA MOJA LA WANA WA ISRAELI WALIAMINI NA TAIFA JENGINE WAKAKUFURU "

(Sura As-saf 61: 15)

Hilo ni kundi la Masihi Isa bin Maryam ambaye ni Masihi wa Musa . Na katika zama hizi ambapo Waislamu wamefarakana , mwamuzi ni Masihi wa Muhammad (saw) ambaye ndiye Mirza Ghulam Ahmad (a. s) Huyu ndie ambaye ametumwa na Mwenyezi Mungu (s w) ukitaka usitake .

MADHARA YA KUMKATAA NABII WA ALLAH

Allah (s.w) anatuma mtume kwa lengo la kuwaogoza watu kwenye njia sahihi . Kuwatoa kwenye giza la upotevu na kuwapeleka kwenye mwanga (nuru) , lakini watu wanapomkataa , hawana salama Allah (s.w) Anasema :

NA ALLAH AMEELEZA METHALI YA MJI ULIOKUWA NA AMANI NA UTULIVU , RIZIKI YAKE IKAUFIKIA KWA WINGI KUTOKA KILA MAHALI, LAKINI UKAZIKUFURU NEEMA ZA ALLAH , KWA HIVYO ALLAH AKAUONJESHA VAZI LA NJAA NA HOFU KWA SABABU YA YALE WALIYOKUWA WAKIFANYA "

(Sura An – Nahli , 16 : 113)

Ayah ii imetaja madhara ya kuzikataa neema za Allah s.w miongoni mwa neema za Allah ni Utume kama tunavyoona katika aya ifuatayo :-

" NA BILA SHAKA ALIWAFIKIA MTUME KUTOKA MIONGONI MWAO , LAKINI WAKAMKADHIBISHA , NDIPO ADHABU IKAWASHIKA HALI WAMEKUWA WADHALIMU "

(Sura Annahli , 16 : 114)

" KISHA TUKAWATUMA MITUME WETU MMOJA BAADA YA MWENGINE , KILA MARA ALIPOWAFIKIA WATU MTUME WAO WALIMKADHIBISHA , HIVYO TUKAWAFUATANISHA BAADHI YAO KWA WENGINE , NA TUKAWAFANYA KUWA VISA , BASI MAANGAMIO KWA WATU WASIOAMINI "

(SURA Al – Muuminuun 23 : 45)

Sisi kazi yetu ni kulingania lakini maamuzi unayo mwenyewe ndugu msomaji wa makala hii na tuko tayari kutoa msaada wakati wowote , Inshaa Allah .

SURA YA TISA
ALLAH YUPA MOJA NASI

Abu Halima akiendelea na shutuma zake ameandika :

" Ukadiani ni harakati za uharibifu na ni mchezo mchafu wa wakoloni , wala hauna mahusiano yoyote na Uislamu " (ukurasa wa 16)

Sisi hatumshutumu mtu yoyote ila pale tunapo shambuliwa , hatuna budi kujitetea.

Kwa bahati shutuma kama

Endelea Uk wa 8..

HATIMA YA WAPINZANI WAWILI WA SEYYIDNA AHMAD[AS]

(SH. MUHAMMAD HUSAIN BATALAWII NA ABDULLAH ATHAM) KUSHINDWA KWA MAADUI

Kutoka Uk 01..

Muhammad saw mashambulio haya yalitumia itikadi zilizotiwa na waislam katika Islam, kadhalika katika hadith za uwongo zilizoingizwa katika vitabu vya kiislamu. Wakati huo mashambulio haya yalifikika hadi ya ubaya wake. Sasa hayako hivi tene. Kwa kuchukizwa sana na upana wa mashambulizi haya, Hazrat Mirza Ghulam as akaazimia kulipa kisasi, matokeo yalikuwa hivi kwamba wakristo walijiona wanashindwa kusimama naye. Waliachilia mbali njia zao za kushambulia. Njia wanayoitumia sasa katika kuandika kuishambulia Islam ni tofauti. Miongoni mwa watukanaji waliokuwa mstari wa mbele kabisa alikuwa Abdullah Atham, aliyekuwa wa kwanza mtumishi serikalini, ilitokea hivi ya kwamba muhadhara kwa kuandika ulipangwa baina ya Hazrat Ahmad na Abdullah Atham. Muhadhara huu ulifanyika Amristhar. Katika mhadhara Abdullah Atham alishindwa vibaya sana. Alidhalilika miongoni mwa wakristo na wengine. "Katika muhadhara huu likazuka suala la miujiza. Kwa suala hili, ilionekana ya kuwa Mwenyezi Mungu hakuuacha muhadhara huu uende bila muujiza. Hazrat Ahmad akapokea ufunuo katika muhadhara upande wa mwongo, ambao umemwacha Mungu hasa na ambao unatafuta kumfanya mtu kuwa Mungu utaangukia motoni.

Hili linatokea mnamo miezi kumi na tano, yaaani mnamo muda unao hesabika kadiri ya mwezi mmoja kwa kila siku moja yamuhadhara huu, kwa sharti kwamba upande wa mwongo usielekee haki." Katika karatasi yake ya mwisho ya majadiliano, hazrat mirza ghulam ahmad alitia bishara hii na akatangaza ya kuwa bishara hii kuwa mtukufu mtume sawa, ambaye Abdullaha Atham alimtaja [mungu apishe mbali] kuwa ni dajjal katika kitabu chake Andruna-i-Bible, [yaan hali ya ndani ya Biblia] alikuwa Mtume wa kweli wa Mwenyezi Mungu.

Bishara hii ilikuwa na sehemu mbili za maana sana;

1. Nikwamba Abdullah Atham (Aliyetafuta kuthibitisha kuwa yesu ni Mungu), atakwenda motoni kwa sababu ya chuki na matusi yake;
2. Kwamba kama atatubia na kutamka kosa lake, atasalimika na adhabu hii. Au kama hakubadili fikara zake na kudumu katika uadui wake na matusi, na kisha asalimike na adhabu hii, bishara hii itakuwa ya uwongo; kwa upande mwingine, kama akijibadilisha na afe tu mnamo miezi 15 kuanzia siku ya mwisho ya majadiliano, hata hivyo bishara itakuwa ni ya uwongo. Maneno ya bishara yameainisha kuwa kwa elimu ya Mwenyezi Mungu, Abdullah Atham ilikuwa aishi umri mrefu zaidi ya miezi 15, lakini ilikuwa afe mnamo miezi 15 kama angeendelea na uadui wake. Kwa kufikiri kidogo maneno hayo yanaonesha kuwa hatua za pili zina adhama zaidi kuliko mbili za kwanza.

Hatua mbili za kwanza ni kwamba kama Abdullah Atham ataendelea na uadui, basi atakufa mnamo miezi 15. Kwani Atham kuendelea na uadui lilikuwa jambo la kawaida kwake na jepesi. Alikuwa mwandishi wa kikristo alieandika kuusaidia ukristo katika kushambulia uislamu. Alikuwa maarufu sana hata miongoni mwa waingereza.

Kwa majadiliano baina ya wakristo na waislamu, alichaguliwa yeye kuusimamia ukristo badala ya mapadre wengine na wahubiri. Wahubiri mashuhuri wa kikristo walikuwa kama wasaidizi wake. Mtu huyu alitazamiwa kuendeleza kushikilia itikadi zake za ukristo. Kwa kufanya yote haya kwa kuueneza ukristo na kuwa msemaji mkubwa katika majadiliano, mtu asingeweza kufikiri hata mara moja angeryudisha nyuma itikadi yake juu ya uungu wa yesu na kuathirika na nguvu za kimwujiza ya uislamu. Kusema kwamba katka hali ile angekufa mnamo miezi 15 inaonekana ni bishara kubwa sana. Lakini Atham alikuwa na umri wa miaka 65 na mtu mzee kama huyu anaweza kusemwa ametumia maisha marefu. Kama angekufa, isngeonekana kuwa niajabu. Bali fikiria sehemu nyingine.

Kama Atham angeacha uadui wake, angesalimika na kifo mnamo miezi 15. Ilikuwa ni vigumu sana kwa Atham kutubia na kuacha mwendo wake kuuadui uislamu. Na kwa kuwa kifo kinaweza kuletwa hata na mikono ya wanadamu, dhamana ya maisha ya miezi 15 haiwezi kutolewa na yeyote. Hatua ya sehemu ya pili ni wazi ilikuwa ngumu sana. Hatua hii iliweza kuifanya bishara kuwa kubwa zaidi na ya kuvutia. Inaonekena ya kuwa Mwenyezi Mungu alichagua sehemu iliyo ngumu sana.

Atham, licha ya umarufu wake na uhodari, aliogopeshwa na bishara hii. Alama yake ya kwanza ilitokea wakati atham katika majadiliano aliweka vidole masikioni na kusema ya kuwa hakumwita mtume saw Dajjal.

Baada ya kutangazwa bishara hii kila mtu akawa anatazamia matokeo yake. Lakini Mwenyezi Mungu hakuacha miezi 15 ipite bila ya alama zingine za kutubia kwa Atham. Atham aliacha kazi zake zote za kuusaidia ukristo. Aliacha kusema na kuandika. Muhubiri mashuhuri na mwandishi hawezi mara moja kuwa kimya kabisa. Hivyo, Atham kufanya hivi, inaonyesha kuwa islamu ilimvutia Atham kwa namna fulani akili mwake, ya kwamba kwa kadiri fulani alifikiri kuwa ni kosa kushambulia, labda hata kupinga dini ya islamu. Lakini hakuonesha hivi kwa kunyamaza tu. Alipata maumivu makali sana ya ubongo, namna fulani ya moto. Mawazo ya uadui kwa islamu yakahama. Alianza kuona ndoto za ajabu na kuzisimulia kwa ndugu na rafiki zake. Aliota juu ya mijoka, mijibwa yenye wazimu, mijitu yenye silaha tayari kumshambulia. Mambo haya hayawezi kuoneshwa kwa mtu kwa njia ya wanadamu. Mijoka na mijibwa haiwezi kutembezwa kwa ajili hii, na katika bara hindi kwa sababu ya marufuku ya kutumia silaha, mijitu yenye silaha isingeweza kuonwa katika safu namna ile. Ndoto hizi zilifanya namna fulani ya moto kwa Atham. Ilikuwa ni matokeo ya mawazo ya toba juu ya kusaidia ukristo katika kuudui uislamu. Moto huu wa ubongo ulikuwa badala ya moto

wa kimwili ambao angeuingia, laiti angeendelea na uadui wake. Kama Imani yake juu ya ukristo ilibakia kama ilivyokuwa kwanza, kama angeendelea kuufahamu uislamu kama dini ya uongo kama alivyo ufahamu hapo kabla, asingetaabika kwa fikara na ndoto za namana ile. Kama aliendelea kuona kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja nae, kwaninin wanyama na wadudu hawa walionekana kwake vya kutisha sana? Kwanini aliacha kuandika kote na kuhubiri kwa niaba ya ukristo? Kwanini alikuwa akienda toka mji mpaka mji kwa hofu?

Kwa ufupi, Mwenyezi Mungu alichagua kutimia kwa sehemu ya pili ya bishara, sehemu iliyo tabiri toba ya Atham. Sehemu hii haikuwa na welekea wa kutimia. Atham akaanza kutia shaka juu ya yesu kuwa mungu. Ukweli wa uislamu ukaanza kuingia akilini mwake. Kwa toba yake mwenyezi mungu alitimiza sehemu ya pili ya bishara hii. Atham alisalimika na kifo ijapo kuwa woga na matisho yalimpeleka karibu yake. Ahadi ya mungu ikawa ya kweli. Alisalimika kwa sababu alitubu.

Hii ilikuwa bishara kubwa sana ya kufaa kufumbua macho ya kila mtu. Lakini kama kusingefanywa chochote baada ya muda ulio tajwa maadui wa Hazrat Mirza Ghulam Ahmad as wangeendelea kusema ya kuwa Atham hakufanya toba yoyote. Ilikuwa ni matengenezo ya Hazrat Ahmad na wafuasi wake.ili kuufanya ukweli wa bishara hii uwe zaidi hata kuliko kwanza, mwenyezi mungu akainua kikundi cha wakristo na waislam kusema ya kuwa bishara ile imethibitika kuwa si ya kweli na ya kwamba Atham hakufa mnamo muda ulio tajwa. Kwa kusema hivi wakaambiwa kuwa bishara hii ilikuwa itimizwe katika moja wapo ya njia mbili. Imetmia katika njia ya pili. Lakini maadui hawakukubali na wakaendelea kusema ya kuwa Atham hakutubia. Hazrat Ahmad as akamwita Atham atangaze kwa kiapo kwamba hao wakristo na waislamu walikuwa wakweli na ya kwamba katika muda wote huu

hakuingiwa na hata chembe ya fikara juu ya ukweli wa islamu na ya uongo wa ukristo. Atham akakataa kutangaza hivi kwa kiapo. Alitoa matamshi bila ya kiapo ya kuwa bado aliufahamu ukristo kuwa ni kweli. Lakni, Alhamdulillah, pale pale akatangaza kwamba Imani yake juu ya uungu wa yesu ni tofauti na Imani ya wakristo wengine. Tangazo hili lilitimiza tu bishara. Kwani bishara ilisema kwa upande uliotafuta kumfanya mtu kuwa mungu utakwenda motoni. Atham alikubali ya kuwa hakumfikiri yesu kristo kuwa mungu. Licha ya tangazo hili, Atham aliulizwa kama atatangaza ya kuwa hakuingiwa na mateso yoyote juu ya ukweli wa itikadi za dini yake nay a kwamba ukweli wa islamu haukumwingia hata chembe nay a kwamba katika muda wote ule aliendelea kuamini yote aliokuwa akiamini hapo kabla. Akimtaka Atham atoe tangazo hili kwa kiapo, Hazrat Ahmad alitangaza kwamba kama Atham akitangaza kwa kiapo kisha asipate adhabu ya mungu, basi yeye ni muongo. Akaahidi pia hapo ya kuwa kama Atham vile kwa kiapo atampa zawadi ya rupia 1,000/- taslimu. Atham akatoa jawabu kwamba kuapa hakuruhusiwi katika dini yake. Hii ilikuwa ni ajabu kwa sababu katika agano jipya wanafunzi wa Yesu wanasemwa walifanya viapo mbali mbali. Katika serikali za kikristo mtu hateuliwi kwa kazi kubwa mpaka awe ameapishwa. Hata mfalme lazima aape. Mahakimu, wabunge, maafisa wakubwa inawalazim kuapa. Kwa kweli mahakama ya kikristo zinasisitiza kufanya kiapo kwa mashahidi wa kikristo. Mashahidi wasio wakristo husema tu, "ninatamka mbele ya mungu wa milele na mwonaji wa milele" n.k.

Kwa hiyo kama kuapa, kwa mujibu wa wakristo, ni haki maalumu ya wakristo, Atham hangeweza kusema si halali katika dini yake. Hivyo kukataa kwake hakukuwa kwa uaminifu. Bali ilikuwa hila na kukwepa kiapo na adhabu zake. Kwani aliona ishara za kutisha hata akafahamu kwa yakini kuwa angekula kiapo, lazima angekufa. Hivyo Atham kukataa kuapa vile kunadhihirisha zaidi kwa kweli ya kwamba miongoni mwa wakristo hakuna kazi yoyote ya maana inayopewa mtu mwingine yeyote mpaka ale kiapo cha utii. Wakristo wa kilutheri, na Atham alikuwa mlutheri, wao huwalazimu kuapa viapo viwili, kimoja cha utii kwa kanisa na kingine kwa serikali. Mambo haya yalipoelezwa kwa Atham alinyamaza kimya kabisa.

Zawadi iliyowekwa na Hazrat Ahmad as kupewa kama angeweza kula kiapo ilipanda kutoka kwenye rupia 1,000/- mpaka rupia 4000/- aliwekewa muda wa mwaka mmoja. Atham angejichukulia zawadi ile kama angeapa. Lakini alijua ya kuwa kwa kuwaogopa watu wa dini yake alikuwa anajaribu kuficha hali ya akili yake aliyo itaabika kweli kwa miezi kumi na tano.

Kwa kujua haya yote hakuthubutu kula kiapo. Akatumia siku zake zote zilizo baki akiwa kimya kabisa.

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

MAJINA YA MWENYEZI MUNGU

Zifuatazo ni sifa, kwa majina zavutia
Kwazo hujiziba nyufa, za shaka mola dhania
Pia hujaza nadhifa, za roho na mwili pia
Wetu mola asokufa, kwasifa ametimia

Kwa allah ninaanzia, sifa zote limebeba
Upweke laoneshea, hakuna wakuliiba
Mwenye kujitegemea, mkwasi asowahaba
Viumbe watajifia, ye milele atakaa

Rahmani mwingi rehema, ulimwenguni kajaza
Hata kabla umba mama, mahitaji lieneza
Hiki pata kwa kulima, na majini kaeneza
Yamama yote rehema, kwake ni moja ya mia

Rahimu wa ukaribu, mfano wake hakuna
Lowapa vyakujikimu, viumbe wanajivuna
Vile alowarehemu, Malipo watayavuna
Jema wanapohudumu, thawabu huwapatia

Maliki wetu mfalme, sisi kwake Tegemezi
Ukubwa wa wake falme, mipaka hijitokezi
Uwezo wa yake falme, ni ule toka wa enzi
arishini ye atame, kila kitu tawalia

Qudus ni mtukufu, kasoro zimemwepuka
Mfano zile za ufu, au uchovu mshika
Au usahaulifu, na usingizi funika
Siku zote mnyoofu, heshima mstahikia

Salamu mwenye Amani, viumbe kuwatuliza
Japo wamo rehemani, hawaachi mchukiza
Hushindania dhambini, visasi kujilipiza
Amani ya Dunia, naya Jannah hutoa

Mlinzi al mu'umin, Imani hustawishia
Huwatia salamani, wale walomridhia
Huchunga zao Imani , shetani sije ondoa
Kwasalama na Imani, wapendwa wake walea

Muhaymin mtunzaji, wakila alichoumba
Napia muangaliaji,Mlinzi wa avo umba,
kwa kudra mwendeshaji, Namna alivoumba
kianzacho mlindaji, mwisho ukifikishia

Alazizi mwenye shani, nguvuze siza mfano
Huoni wake mwishoni, eti shiindwa mashindano
Awekalo ukumbini, halitoki kwa mkono
Wala kwa nguvu ya jinni, bila yeye kuridhia

Jabbari nguvu kajaa, mambo kurekebishika
Kilicho jivunjikia, kwake hutengezeka
Kilochojipungukia, kwake hukamilikika
Nguvuze zilizojaa, hakuna cha kupimia

Mutakabbir mkuu,ukuu wote niwake
Vyazihirisha ukuu, vile vitokavyo kwake
Kila kitu cha ukuu, yeye yupo juu yake
Mutakabbir mkuu, heshima yamfalia

Khaliq mwenye kuumba, ameumba kila kitu
Vyakuoneka kaumba, toka kwa kisicho kitu
Visooneka kaumba, toka kwa asojua mtu
Siri pekee kuumba, ni yeye anatambua

Al baar tengeneza, baada ya kukiumba
Kilichopo kisawaza, kukipatia na umbo
Kiloumbwa tengeneza, Kwa mwili nayo maumbo
Al baar muundaji, vile alojiumbia

Musawwir vipatia, viumbe zakwao sura
Atakalo hulipinda, mraba au duara
Huchagua nalopenda, endane na ile sura
Umbile takalounda, fanana nayo tabia

Kwajina alghafari, husamehe nakubali
Madhambi yalodhihiri, nahata yale ya siri
Zenye kujaa bahari, hata za kwenye bakuri
Usamehe walokiri, wepusha adhabu kali

Kahhari mwenye uwezo, kila kitu kazunguka
Hakuna kwake kikwazo, atakapo tamka
Toroka wake uwezo, katu hatotorokeka
Haihitajiki nyenzo, uwezoe utambua

Wahab mwenye kutoa, hakuna hujaza kitu
Huotesha na mimea, pakame paso nakitu
Alokosa jipatia, yeye humjaza vitu
Wahabu mwenye kutoa, atakaye mpatia

Razaki wa kuruzuku, mwenye kutoa riziki
Viumbe mithili kuku, bila yeye hakiliki
Huziandaa za siku, viumbe zao riziki
Haachi kuturuzuku, tutendapo maasia

Fataha mfunguaji, wajambo nakuanzia
Pia ni muondoaji, tatizo sijetokea
Napia mzuiaji, madhara kutuvamia
Fataha mfunguaji, mwishomwema hujalia
Al alim mjuzi, mwenye kuyajua yote
Mambo yote mtambuzi, hakifichiki chochote
Humpatia ujuzi, amtakaye yeyote
Tuombe ujuzi kwake, kila fani na elimu

Qabidhi mwenye vikwazo,mitihani hututiaa
Jaribu wetu uwezo, wasubira vumilia
Hutupima kwa tatizo, lililo nasi sawia
Heri na shari ni vyake, nafusi kuzipimia

Basiti ni mwondoaji,washida napotokea
Pia yeye mwenezaji, furaha jonzi ondoa
Tena mrahisishaji, ugumu napotokea
Nafuu hutoka kwake, shida zikikwelemea

Khafidhu hulainisha, na pia hunyenyekesha
Nafusi anazishusha, ,Kwa mola zilainisha
Au kujinyenyekesha, yule alompandisha
Unyenyekevu ni kwake, amtakaye humpa

Raafiu mnyanyuaji, na vyeo ni mtoaji
Tena ni mtakasaji, madaraja mgawaji
Yeye pia mpangaji, ngazi mkadiriaji
Vyeo vyote Toka kwake, hunyanyua na kushusha

Al muizu humpa, heshima amtakaye
Na heshima akikupa, hakuna aondowaye
Hata kibaki mifupa, takuwa heshimiwaye
Heshima hutoka kwake, humpa amtakaye

Mudhilu huzalilisha, yeyote amtakaye
Akisha kudhalilisha, hakuna aondowaye
Hadi kijirekebisha, ndipo uwe radhi naye
Udhalili hutoka kwake,waovu hudhalilisha

Samiu wakusikia, tena msikivu sana
Chumbani jinong'onea, yeye kwake ni bayana
Maombi huyasikia, yawazi nayo fichana
Maombi yaende kwake, asikia paka sasa

Basir mwenye kuona, hakifichiki chochote
Nje ndani anaona, pia kila pande zote
Kikubwa kidogo ona, sipunje Wala mkate
Nihakijifichi kwake, lolote tunalifanya

Hakam mwenye hukumu, hakuna kupendelea
Yeye ndo wetu hakimu, kwa adili hukumia
Kwani anayo elimu,yayote yanotokea
Hukumu sawa ni kwake, ya viumbe huitoa

Al adli mwadilifu, katika viumbe vyake
Hupenda uadilifu, tendee viumbe wake
Baada ya wetu ufu, hukumu tatoka kwake
Haki inatoka kwake, tuombe uadilifu

Latifu mwenye uzuri, na mpole kila hali
Mjuzi wa kila siri, za uzuri mbalimbali
Tuvionavyo vizuri, ni haba ya yake hali
Uzuri upole ni wake, viumbe wamegawiwa

Khabir mwenye habari, ya kila tukionacho
Pia mjuzi wa siri, wa vyote vilivyo ficho
Humpa zake habari, amchaguaaye kwacho
Kila Siri ni ya kwake, humjuza mtakaye

Haliim muda hutoa, wa watu kubadilika
Kabla hawajajutia, adhabu takapofika
Nafasi hutuachia,yatoba kupokeleka
Huruma yote ni yake, kidogo tuliyopewa

Adhiim alotukuka, ukubwa ametimia
Kwa macho hatooneka, kwa ngozi hatohisika
Kwa yeye kutambulika, ni kwa sifa tamjua
Utukufu ni wakwake, apasaye kusifiwa

Ghafur husamehea, yote makosa kwa watu
Pia hutuzuilia, tokeo makosa yetu
Hachoki tusamehea, kirudia dhambi zetu
Usamehevu ni kwake, tuombe atuzuwiye

Shakur mshukuriwa,vizuri mwenye kutoa
Yeye ndo wakusifwa, viumbe lowapatia
Sifa njema mejaliwa, kasoro memwepukia
Shukrani zote ziwe kwake, tushukuru tulopewa

Masihi Omary Stambuli Kisagwa
Litaendelea…. Inshallah toleo lijalo

BURIANI

Moshi bini Mohammedi, daima tutakumbuka
Kwa ile yako juhudi, maohubiri kupeleka
Si vijiji si biladi, huko kote ulifika
Kuufikisha ujumbe, amedhihiri Masihi.

Karibu hata baidi, na kote ulizunguka
Kuipeleka Zawadi, ilotoka kwa Rabuka
Hidaya hiyo Mahadi, wa Mtume msifika
Ukawapa Ushahidi, wa yote uliyosema.

Kufaulu ukazidi, muhadhara wa Nguruka
Ulileta mashahidi, Masheikh walosifika
Na Qur'an Majidi, ndiyo iliyotumika
Wakabaki vinywa wazi, Maulam awa Kigoma.

Tama twaomba Wadudi, Aweze kusitirika
Bustani ya waridi, nzuri ilopambika
Kwa manukato na udi, na mito kutiririka
Malipo ya watu wema, walotimiza wajibu.

Na Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

FUNZO KATIKA MAISHA

Mtu mmoja alikuwa na wana wanne. Alitaka wanawe wajifunze kutohukumu mambo haraka-haraka. Kwa hiyo akawatuma kila mmoja katika mgawo fulani, kwa zamu waende kutazama mti wa peari uliokuwa mbali sana.



Mwana wa kwanza alienda katika msimu wa baridi wa pili katika msimu wa spring wa tatu katika msimu wa majira ya joto na mdogo katika vuli. Walipomtembelea wote na kurudi, mtu huyo aliwaomba wanawe wamweleze jinsi mti huo ulivyokuwa.

Mwana wa kwanza akasema, "Mti huo ulikuwa mbaya, umepindika na kupotoshwa" Mwana wa pili akasema, "Hapana, ulikuwa umefunikwa na umejaa ahadi" Mwana wa tatu hakubaliani na ndugu zake na akasema, "Ulikuwa umejaa maua yenye harufu tamu na ulionekana kuwa mzuri sana" Mwana wa mwisho, mwana mdogo hakubaliani na wote na akasema, "Mti ulikuwa umeiva na matunda, umejaa maisha na utimilifu".

Kisha mtu huyo akawaambia wanawe kwamba walikuwa sawa, kwa sababu kila mmoja aliona mti huo katika misimu tofauti.

Aliwaambia kwamba hawawezi kuhukumu mti, au mtu, kwa majira fulani tu. Kiini chao ni raha, furaha na upendo unaotokana na maisha unaweza kupimwa tu mwishoni, wakati misimu yote imekwisha.

Kama wewe ukihuzunika kwa sababu ya msimu mmoja hautapata ladha ya msimu mwingine., uzuri wa majira ya joto na kutimiza kuanguka kwako. Aliwaambia wasiruhusu maumivu ya msimu mmoja yaharibu shangwe ya misimu mingine yote.




Mafundisho:

Usihukumu maisha kwa msimu mmoja mgumu, uvumilie kupitia vipande ngumu na nyakati bora hakika zitakuja baadaye.



Unganisha Nukta kupata Mchoro



JINSI YA KUPIKA KUKU WA MCHUZI

MAHITAJI

- Vipande vya kuku (Unaweza kuwa na idadi yeyote, kutegemea na walaji)
- Mafuta ya kukaangia
- Chumvi
- Pilipili manga
- Kitunguu saumu cha unga
- Tangawizi ya unga kijiko 1 cha chai
- Limao 1
- Pilipili hoho 2
- Kitunguu maji 1
- Karoti 2
- Nyanya au tomato paste
- Binzari au chochote unachopenda kuweka kwa kuleta ladha



MAELEKEZO

•Kwa kawaida imezoleka kuanza kwa kuchemsha kuku,halafu tunamkaanga.Leo tutatengeneza hiki chakula tofauti kidogo

•Tutaanza kukaanga kuku halafu tutakuja kuwapika kwenye mchuzi mzito wa nyanya na mbogamboga.

•Ladha tamu ya viungo na kuku vinafanya hii supu kuwa maridadi na raha kabisa kuila kwa mchuzi.

•Andaa kuku,kata vipande unavyoweza kula,osha vizuri na weka pembeni. Usiwatoe ngozi,ili isaidie kuiva vizuri.Ngozi huiva vizuri wakati wa kukaanga.

•Weka viungo kwenye kuku,Limao,chumvi,kitunguu saum,tangawizi na pilipili manga.

•Acha viungo viingie vizuri kwa muda wa dakika15 hadi 20.Unaweza kuacha zaidi lakini si lazima sana.

•Weka mafuta jikoni kwenye chombo kinachotosha.Acha yapate moto vizuri,kisha weka vipande vya kuku.

•Acha kuku waive vizuri hadi wakauke na kubadilika rangi.Inachukua kama dakika 10 hivi.

•Toa kuku na weka kwenye tissue paper,
ili wachuje mafuta vizuri.Rudia hatua hii kwa vipande vilivyobaki.

•Andaa nyanya (au kama una tomato paste ni vizuri pia), pilipili hoho na karoti wakati kuku anaendelea kukaangika vizuri.

•Kuku akishaiva,bandika kikaangio au sufuria iikoni.

•Weka mafuta ya kula kiasi,acha yapate moto.Weka kitunguu,acha kiive na kilainike.Weka nyanya,koroga na acha ichemke kiasi hadi zilainike.Weka karoti na pilipili hoho.Funika acha zipate kuiva kiasi.

•Weka vipande vya kuku unavyotaka kuvipika.Koroga vizuri.Ongeza binzari au mchuzi mix upendayo ili upate kuleta ladha zaidi.

•Koroga vizuri acha kati ya dakika 5 hadi 10 ili vipate kuivia na kuleta ladha nzuri

•Ukimaliza unaweza kutoa na kuacha ipoe au
ukala moja kwa moja na chakula chako ugali,wali

MAJIBU KWA MASALAFI

Kutoka 04

hizo ambazo Abuu Halima anatushutumu , wanashutumiwa pia hao masalafi ambao ni Mawahabi kwa jina lengine . Soma haya :

" Kwa maana hiyo , Mawahabi ni picha halisi iliyotengezwa na Waingereza ili kubomoa mshikamano wa Waislamu "
Rejea (Upotofu wa madhehebu ya Uwahabi / Ansawr Sunna uk 90)

Tukiachilia mbali majisifu na majigambo , Jumuiya ya Waisalamu WAAHAMDIYYA NDIYO Jumuiya pekee yenye mipango madhubuti ya kuleta ushindi katika Uislamu . Kwanza kabisa tunaye kiongozi , kinyume na Waislamu wengine wote.
Kiongozi wenyewe ni KHALIFA chini ya misingi ya UNABII.
Kama alivyoeleza Mtume (saw)
"Unabii utakuwepo kati yenu mpaka Allah atakapopenda atauondoa , Kisha utakuwepo kati yenu ukhalifa chini ya misngi ya Unabii , Kisha utakuwepo kati yenu ufalme wa kuudhi mpaka Allah atapopenda , kisha utakuwepo kati yenu ufalme wa Kijeuri , Kisha utapatikana UKHALIFA chini ya misingi ya UNABII . Kisha akanyamaza "
Rejea (Mishkat , na Musnad Ahmad babu indhar j .4 uk 253)
Baada ya Mtume (saw) kufariki . Ulifuata Ukhalifa chini ya misingi ya Unabii – Hao ndio :-
Hadhrat Abu Bakri Swiddiqq (r .a) Hadhrat Umar bin Khattwaab (r. a) Hadhrat Uthman bin Affan (r. a) na Hadhrat Aly bin Abi Muttalib (r.a) .

Kisha ulikuja ufalme wa kuudhi na kisha ufalme jeuri wa akina Hajjaj bin Yusuf.
Falme hizo Allah (s.w) ameshaziondoa , hazipo . Ndipo Allah (s.w) akamtuma Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad , Masihi aliyeahidiwa na Imam MAHDI (a.s) ambaye alianzisha Jumuiya ya Ahmadiyya mnamo mwaka 1889. Alifariki mwaka 1908 ambapo ulianza rasmi UKHALIFA chini ya misingi ya UNABII , na ndio unaendelea . Wako Waislamu wanaohangaika kumska khalifa wakidhani labda khalifa huyu wa kuwaongoza Waislamu wa dunia mzima watampata kwenye makongamano , yaguju . Njia pekee ya kupatikana kwa khalifa huyu imeelezwa katika surat – annur Allah (sw) anasema :

"ALLAH AMEWAAHIDI WALE WALIOAMINI MIONGONI MWENU NA KUFANYA VITENDO VIZURI , BILA SHAKA ATAWAFANYA MAKHALIFA KATIKA ARDHI KAMA ALIVYOWAFANYA MAKHALIFA WALE WA KABLA YAO , NA KWA YAKINI ATAWAIMARISHIA DINI YAO ALIYOWAPENDELEA , NA ATAWABADILISHIA AMANI BAADA YA KHOFU YAO .WATANIABUDU , HAWATANISHIRIKISHA NA CHOCHOTE ....."

(Surat - annur 24: 56)
Maana yake ni kwamba :
1.Allah (sw) mwenyewe ndie atakaechagua makhalifa hao na sio vikao .
2. Kazi ya makhalifa hao ni kuimarisha dini hii ya Kiislamu.
3. Hata umati uliopita wa Banii – Israil ulijaaliwa Makhalifa baada ya Nabii Mussa (a. s)
4.Makhalifa hawa wa Kiislamu watafika katika zama ambapo Waislamu wamo katika shida kubwa ndipo Allah (sw) atawaimarisha kupitia hawa makhalifa .
5.Makhalifa hao watafanya kazi ya kuondoa shirki ambayo itakuwa imetapakaa miongoni mwa Waislamu na watu wengine .
6. Yeyote atakyewakataa makhalifa hawa atahesabiwa kuwa amevunja amri ya Allah (sw) .
Neno la kiarabu lililotumika ni Al-fasikun ambalo tafsiri yake nyengine ni wahuni .

Ukhalifa wa Kiislamu ulianza mara baada ya kufariki Mtume (saw) lakini ulidumu kwa muda wa miaka thelathini kasha ulikatika . Lakini ahadi hii iliendelea kuwepo hadi muda ataodhihiri Masihi aliyeahidiwa ambapo muda wenyewe ndio huu . Tunaofaidika na ukhalifa huu ni sisi wa Ahmaddiyya kwa vile Waislamu wengine wamefunga utume na ukhalifa haupatikani bila utume kwanza kama tulivyoona katika hadithi ya Mtume (saw) iliyopo kwenye sura ya tisa ya makala hii .
Neema nyengine Allah s.w aliyotujaalia ni udhibiti wa mapato na matumizi kutokana na mfumo ulio mzuri , chini ya Khalifa wetu[atba] Jumuiya yetu inajitegemea, haihitaji ufadhili wa mtu au taasisi yoyote.
Alhamdullilaah . Hata Abu Halima ameliona hili na ameandika :
" Moja ya kazi muhimu wanazofanya Makadiyyani ni kujenga misikiti na shule " (uk.6)
Lakini jambo jingine la

Itaendelea toleo lijalo Inshallah

MATUKIO KATIKA PICHA

WAHITIMU - SHULE YA MSINGI AHMADIYYA WAFANYA MAHAFALI YAO



mafanikio na maendeleo ya shule, na akaeleza kuwa mahafali haya ni yatano na jumla ya wahitimu kwa miaka hiyo ni 121 (mia moja na ishirini na moja) ambapo wahitimu wa mwaka huu ni 28.

Aidha kwa upande wake Afisa elimu kata aliwaondoa hofu wahitimu ya kuwa kwa maandalizi mazuri waliyo yafanya watafaulu vizuri.

Naye Mkurugenzi wa shule Maulana Sheikh Abid Mahmoud Bhatti sahib Naibu Amir na Principal Jamia Ahmadiyya Tanzania alieleza ubora wa elimu itolewayo na shule hiyo na kusema kuwa amefanya utafiti wa kutosha na kugundua kuwa wanafunzi wote wanao toka hapo kwenda secondary school wanafanya vizuri sana kwa upande wa masomo na nidhamu.

Aliwataka wahitimu hao kutofanya udanganyifu wa namna yoyote ile katika mitihani kwani waalimu wao wame waandaa



vizuri sana kwa jukumu hilo. Kisha alimkaribisha Mgeni rasmi ili kugawa vyeti kwa wahitimu na kutoa nasaha kwa wahitimu na hata kwa wageni waalikwa.

Katika nasaha zake Mheshimiwa Amir sahib Aliwapongeza wahitimu kwa kufikia hatima hiyo na kuwataka wasibweteke, bali waongeze bidii zaidi kwani wame maliza hatua ya kwanza na sasa wanaenda kwenye hatua zifuatazo ambazo ni ngumu sana. Aidha Amir sahib aliwataka wazazi na walezi wa wahitimu hao kuwasimamia vizuri Watoto wao ili waweze kutimiza ndoto zao, bali aliwashajiisha wahitimu wajitahidi sana na kumtanguliza MwenyeziMungu kwa kuomba msaada kwake ili waweze kufikia daraja za juu kabisa katika elimu.

Mwisho Amir sahib aliongoza maombi ya kimya na kumaliza hafla hiyo na kisha wahitimu, wazazi na wageni waalikwa walishiriki katika chakula cha pamoja,







SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka Uk.12

wote tumeshiriki Jalsa salana hii. Siku tuliyokuwa tunaondoka kuja Qadian nilikutana na Mzee Ramzan Fazal ambaye alishiriki Jalsa Salana 2023 Qadian akiwa pekee yake kama mtanzania, na akanieleza kuwa maombi yake yamekubaliwa kwa sababu alifanya maombi maalum kuwa Mwenyezi Mungu awezeshe watanzania wengi kuhudhuria Jalsa Salana Qadian, nashukuru kuwa mmoja wa ukubalio wa maombi yake. Jalsa salana Qadian mwaka huu ni Jalsa ya kwanza kuhudhuriwa bila ya Madarwesh, kwani Darwesh wa mwisho tulimzika wiki mbili kabla ya Jalsa Salana, moyo wangu ulikuwa unaona ni kana kwamba ni ukurasa mpya katika maisha ya jumuiya bila ya wale ambao walipigana kwa jasho na damu kuihami Qadian na Jamaat kwa ujumla.

Mukarram Tayyib Ali Sahib Darwesh ninazo kumbukumbu zangu binafsi kwa mda mfupi huu kumhusu yeye kwa mwezi mmoja kasoro tulioshi Qadian kabla ya mauti yake, alikuwa analetwa msikitini kila siku na kiti chake cha magurudumu na kukaa nje ya geti la msikiti, na waliotusimulia walisema kuwa yeye alikuwa mlinzi wa msikiti hivyo alipenda kukaa pale na kuona jinsi watu wanavyoingia msikitini na kutoka hivyo kila siku tulikuwa tukipita na kumsalimia kabla ya sala na kutoka msikitini. Kuna matukio mawili nayakumbuka mno niliyoyashuhudia kwake.

Omba omba wa India ni wasumbufu mno, mimi walishanitoka rohoni kiasi Fulani nikisema sitaki kuwapa hela tena mpaka nijisikie mwenyewe kutoa. Hivyo siku moja nilikuwa natoka msikitini nikamuona ombaomba mmoja amesimama kando yake na yeye akiwa amekaa kwenye kiti chake, mara kadiri nilivyokuwa natoka kuelekea getini nikaona ametoa noti na kumpa Yule omba omba japo omba omba labda macho yake yalikuwa ni kwa wale wanaotoka getini msikitini hivyo hajamuona Tayyib Ali sahib akimpa ile noti, hivyo ilibidi amuambie kwa sauti 'Ye loo' kwamba chukua hii, ile mandhari ilinipiga moyoni vibaya, nikijiuliza mzee huyu amekaa chini lakini anatoa lakini mbavu nzima mimi nina nguvu na kutembea sitoi kisa kero, nilijitathmini mno na kubadili msimamo wangu.

Tukio la pili ilikuwa natoka msikitini muda wa adhuhuri nikamuona amekaa katika kiti chake akiwa kimya mno, ilikuwa ni kawaida yake kukaa kimya, basi nikaenda kumpa mkono kumsalimia, lakini hakupokea nilivyosimama kwa sekunde kadhaa nikagundua anasali, niliathirika mno na hali yake ya uzee lakini bado anasali sala zake na hali yake ile, alikuwa mwembamba mrefu na athari za uzee zilikuwa zinaonekana usoni mwake lakini Mwenyezi Mungu alimpa nguvu ya kusali mpaka mwisho.

Sheikh Hussein Yusuph Ng'amilo amenisimulia kuwa aliona ndoto asubuhi ya siku ambayo Tayyib Ali sahib alifariki kwamba amesimama mbele ya Tayyib Ali Sahib na anasalisha sala ya jeneza, na anasema alipoenda kusali sala ya adhuhuri alimuona sehemu ile ile anayokaa na baada ya magharibi ndipo alizidiwa na kufariki. Mazishi yake yalikuwa ya namna yake, kila mtu alipewa nafasi ya kumuuona mwili na kuuaga kabla ya kusaliwa, na kama hivyo vijana wa Afrika tulikuwepo kwa ajili ya kumsalia na kumzika.

Mazishi yake hayakuwa ya kawaida kwani nimehudhuria jeneza kadhaa na utofauti niliushuhudia, kwani Tayyib Ali sahib alizikwa kwa zaidi ya masaa mawili, na kila mtu aliyehudhuria alipanga mstari kuweka mchanga kaburini mwake na wazikaji walikuwa huru kabisa kumuacha kila mtu kuchukua nafasi hiyo, kichwani nikijielezea kuwa kuna kuzikwa na kufukiwa.

Roho huacha dunia, Furaha hutanda kwao
Zipo dunia hufia, Kahara alama yao

Jalsa salana Qadian ilikuwa ya kihistoria mno, ilirudisha saa nyuma na kuandika historia upya, Jalsa salana ilianzishwa 27 Dec 1891 na ilifanyika katika Masjid Aqsa Qadian kwa mara ya kwanza, na mwaka huu pamoja na maandalizi yote kukamilika lakini ilinyesha mvua ya ghafla na kufanya siku mbili za jalsa kurudi kufanyika katika Masjid Aqsa yaani 27 -28 na ndizo siku ambazo Saydina Ahmad (as) alifanya Jalsa salana pindi ilipoanzishwa, lakini mwaka huu kwa shani kubwa na kwa ukubwa mno, kwani wanaume wote tuliyohudhuria Jalsa tuliweza kukaa katika msikiti wa Aqsa na kufanya jalsa huku wakina mama wakiwa katika msikiti wa Masjid Anwar huku tukiunganishwa na MTA India kuangalia Jalsa katika kumbi zetu na kuifuatilia, binafsi siku ya kwanza nilishafika ukumbini kabla ya mvua kuanza mara mvua iliponyesha tulijifunika turubai za nailoni kabla ya tangazo kufanywa kwamba wote tuelekee Masjid Aqsa na Jalsa itaendelea huko mpaka hali ya hewa itakapo kuwa sawa.

Siku ya mwisho ya Jalsa salana ambapo Huzoor anwar (aba) anahutubia wahudhuriaji wa Jalsa salana Qadian moja kwa moja kutoka London ni siku ya kipekee mno, hali ya hewa ilitengemaa vyema mno, na ukumbi wote uliwekwa viti kwa sababu mazulia yote yalikuwa yamelowa na ilikuwa ni tahadhari kwamba kiti unaweza kukaa hata wakati wa mvua, lakini mtu akikaa chini maji yakianza kujaa atalazimika kusimama.

Alhamdulillah Mwenyezi Mungu aliifanya siku hii kuwa maalum sana, upande wetu ilikuwa maalum sana kwani ilikuwa ni mara ya kwanza kufanya mkutano na Huzoor (aba) kupitia njia ya video lakini pia tukiwa katika ardhi takatifu ya Masihi aliyeahidiwa (as).

Ndugu zangu walikuwa na shauku kubwa sana ya kuimba shairi mbele ya Huzoor (aba) ili kuwakilisha Afrika katika mwisho wa Jalsa Salana, lakini mchakato wake ulikuwa mrefu mno na hawakufua dafu na wengi walibaki na makasiriko, lakini Mwenyezi Mungu aliandaa nafasi muhimu zaidi kwa WaAfrika kwani siku ile nchi kadhaa zilikuwa zinamaliza Jalsa salana yao, baada ya watu wa Qadian kumaliza mashairi yao na Huzoor (aba) kusalimia na kuanza kuondoka, walinzi walimpa ombi kuwa waafrika wanataka kuimba, Huzoor (aba) alirudi na kuanza kusikiliza mashairi kutoka Afrika na kuunganishwa

Ukurasa wa 11

SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Kutoka uk. 11

na MTA moja kwa moja, kwangu ni kitendo kilicho nitoa machozi mpaka mwisho, furaha yangu ilizidi mipaka, kwa sababu nilikuwa nimejifunika skafu usoni nilikuwa huru kutitirisha machozi yangu na mpaka nilikuwa natetemeka mwili kabisa. Tulipomaliza Jalsa Salana siku ile ile nilimuambia Maulana Tahir Marunda kuwa dua zimekubaliwa na waafrika wamepata nafasi kubwa zaidi mbele ya Huzoor (aba).

Kipindi cha mwisho kinakuwa muhimu mno watu wote wanakimbilia eneo la kijani ili kupata urahisi wa kumuona Huzoor (aba) na pia kuonwa na Huzoor (aba) kwani ndio eneo ambalo kamera zinapita mara kwa mara.

Maandalizi ya Jalsa salana Qadian yanaanza siku kumi na tano kabla ya Jalsa salana yenyewe, taa za mapambo zinawekwa wiki mbili kabla na Jalsa gah inaanza kuandaliwa, Wanajumuiya wa Wakashmir ndio wanaofanya kazi nyingi za Jalsa salana, kwani wao wiki mbili kabla wanawasili Qadian na kuondoka Qadian baada ya kumaliza kazi zote za kurejesha kila kitu mahali pake. Takriban vijana mia tano wa kikashmir wanafanya kazi zote za Jalsa salana, kuanzia ulinzi usiku na mchana, kuosha vyombo, upishi, usafi n.k. wao wanakaa kwenye mahema siku zote za Jalsa salana hawajali baridi wala shida zozote za hali ya hewa. Wana asili Fulani ya ukali na kutokujali shida, mtu akileta shida wanamshughulikia vizuri kwa sababu baada ya Jalsa wanarudi makwao namaanisha kwamba sio watu wenye asili ya Qadian, lakini hakuna visa vya hatari kuhusu isipokuwa jazba yao ya kujitolea, kwamba ndio wakwanza kufika Qadian kwa ajili ya Jalsa na wa mwisho kuondoka.

Ukiondoa nguvu kubwa ya wanajamaat wenyewe kama hivyo lakini bado wapo wanaopata nafasi ya kuajiriwa katika siku hizi za Jalsa Salana kuendesha kazi mbali mbali, mfano sisi wakati wa Jalsa Salana tulihamia Sara –e-Ubaidullah (Mauritius guest house) ambapo pale kulikuwa na wafanyakazi watatu wa kulipwa ambao sio wanajamat walikuwa wanafanya kazi ya kufua, kusafisha vyumba, na kuandalia wageni vyakula lakini hapo pia kulikuwa na wanafuzi wa Jamia takriban watano wanaoratibu na kufanya kazi zote za kuhakikisha wageni hawapungukiwi chochote.

Na kwa siku wale ambao wanahudumiwa wanalipwa Rs 500, baada ya Jalsa Salana utaona watu wengi katika ofisi ya Jalsa ili kuchukua fedha zao za kuhudumia Jalsa Salana, yaani wale ambao wanatoka nje ya Jamaat.
Alhamdulillah hotuba zote za Jalsa Salana, darasa za asubuhi, na mashairi yaliyoimbwa na nidhamu yote ya Jalsa Salana ilikuwa ni jambo la kujifunza mno na kuelimisha na kukamata jazba ya mtu.

Hapa Qadian kila kitu kinaandaliwa mapema na kupelekwa kwa Huzoor anwar (aba), yaani hata mashairi yanarekodiwa na kupelekwa kwa Huzoor (aba) ndipo yanapata ruhusa ya kuimbwa mbele ya hadhara ya Jalsa, na waongeaji wote wanakuwa wamepata ruhusa kwa Huzoor Anwar (aba) pamoja na kitu wanachoenda kukiwasilisha, ndio maana kupata nafasi katika Jalsa Qadian hata ya kuimba shairi ni muhali kwani kila kitu kinakuwa kimeshapangiliwa mapema na kuhakikiwa.

Majukumu ya Khuddam ul Ahmadiyya katika shughuli zoteza Jamaat hapa Qadianni mapana mno, kuanzia ulinzi mpaka katika shughuli za mazishi zinapotokea zote ni shughuli zao. Nilichojifunza ni kwamba hapa wenzetu hawahitaji kundi kubwa la khuddam ndipo wafanye jambo Fulani, laa hasha! hao hao wanaopatikana wakati huo basi wanalifanya jambo na kuwawakilisha wengine, mfano nilieleza nimewahi kuchezesha mechi ya Khuddam waqf-e-nou katika mashindano yao kuelekea Ijtimaa yao, walikuwa wanne wanne tu kila upande wakacheza na wakakusanya matokeo, na hata vikao vyao wanafanya baada ya sala Fulani msikitini na kuamua mambo yao, hivyo basi si jambo la kuvunjika moyo au kutokufanya jambo kwa sababu mahudhurio ni machache bali ni namna gani tunaweza tukatumia nguvu kazi iliyopo wakati muafaka.

Tumepata nafasi nzuri ya kuona maisha ya Qadian ya kabla na baada ya Jalsa, kipindi ambacho barabara za Qadian zilibadilika kuwa soko kubwa na baada ya hapo kurudi katika hali yake ya kawaida.

Jalsa Salana kwa wenyeji wa Qadian na hata watu wanaotoka nje ya Punjab inakuwa ni msimu wa kuvuna, na wengi baada ya Jalsa salana kuisha wanafunga maduka na migahawa yao kwa muda kabla ya kurudi tena katika biashara. Mandhari hii imenisaidia mno kimawazo na taswira ya Qadian, kwani unapoondoka katika sehemu ambayo ilikuwa na tukio Fulani kabla ya tukio kuisha basi taswira inayobakia kichwani ni lile tukio tu na mandhari yake, hivyo hapa kichwani mwangu naiona Qadian ikiwa safi na mitaa yake yote.

Katika kipindi tulichokuwa tunasubiria tarehe zetu za kurudi nyumbani tumepata kukaa na maulamaa tofauti walioitumikia Jumuiya muda mrefu na kustaafu na kupata nafasi ya kuuliza maswali na kupata majibu kutoka kwao, ilikuwa ni kipindi cha kama una jambo linalokutatiza basi unaenda tu unauliza na kupata ufafanuzi wake. Nilichukulia wakati huu kama wakati wa kumalizia masaza ambayo yalikuwa bado yamebakia, wenye kufunga kwa ajili ya shukurani walifunga na kuweka ratiba mbali mbali, wengine ambao majibu ya maombi yalikuwa bado basi ilikuwa ni muda muafaka wa kuomba tena kwa ajili ya majibu yake, kwani kipindi cha Jalsa Salana Dar ul Masih ilikuwa huwezi kupata nafasi ya kwenda na kufanya maombi mda mrefu hasa kwenye Baitul Dua na sehemu nyingine, lakini baada ya Jalsa Salana fursa ilikuwa pana mno ya kwenda mda unaotaka na kuomba dua yoyote ile, na kama unataka kuona raha ya Qadian basi uende wiki tatu kabla ya Jalsa Salana au urudi wiki tatu baada yake.

Allah atujaalie kupitia safari hii ya Qadian, tuweze kujifunza na kunufaika kwayo, Amin.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi Yangu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE







SAFARI YA QADIAN, UZOEFU NA HALI ZETU

Na.
Sheikh Shaban Othman Shunda




Ndugu yangu Faizan Ramzan Fazal Madhwan alitukuta huku, Yeye alikuja kwa ajili ya rukhsitana yake na walima wa ndoa yake, hapo kikundi cha walaji na wapenda kula kikatimia, bwana Faizan ametutoa nje mara kadhaa kwa ajili ya chakula, tumekula sehemu mbalimbali na migahawa ya Qadian. Lakini kikubwa zaidi ni sherehe ya rukhsitana yake na walima ambayo pia tulialikwa kama ndugu wa bwana harusi na tukazifanyia uadilifu sherehe hizo.

Binafsi yangu napenda sana kusoma kupitia ndugu zangu, nilichojifunza kwa Faizan tangu mchakato wake wa kuoa India unaanza, ni kwamba unapohitaji kitu fulani basi ni lazima ujitolee na kujitoa kwa ajili ya kitu hicho, ni mdogo wangu lakini nimemuona kichwa chake na kifua chake ni mtu mwenye maono ya mbali na subira ya hali ya juu. Na anaamini katika uwekezaji wa maombi na raslimali, ni kana kwamba jambo lake halifanyi kwa ajili yake mwenyewe bali kuna msukumo fulani ndani yake ambao unamwambia fanya jambo hili linafaida baadaye naye anafuata maelekezo tu. Ni rafiki yangu mno na nimejua kwanini anaweza kufanya biashara Kariakoo kupitia hili. Na mara nyingi watu wa hivyo ni kuwaombea tu juu ya mambo yao na kuwasikiliza wanachotaka kwani ushauri wa tofauti na maamuzi yao haufanyi kazi na wala mawazo yao hayabadilishwi na kitu chochote, kwani wanayaona matokeo yao usoni kabla ya kuwafikia.

Jalsa salana Qadian 2024 ilikuwa ya kipekee mno hasa kwa historia ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania, kwa mara ya kwanza watu saba kutoka Tanzania wamehudhuria Jalsa salana Qadian kwa pamoja, japo kuwa kana kwamba watu wawili ndio walikuja maalum kwa ajili ya Jalsa salana yaani Mwalimu Omari Mnungu na Bwana Salehe Yaasin sahib, kwa namna yoyote

UK. 10



Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,000/=.

Je, Wajua?

Kiichiro Toyoda ndiye mwanzilishi wa kampuni ya Toyota Motor Corporation na Toyota group ya magari. Inamiliki kampuni tanzu nyingi, zikiwemo Daihatsu, Hino motors, Lexus.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com